# NJIA BORA ZA USIMAMIZI WA MGAWANYO WA MAPATO NA FAIDA MBALIMBALI ZITOKANAZO NA MKUHUMI TANZANIA

**AUGUST, 2014**

**KIJITABU HIKI KIMETOLEWA NA MRADI WA MGAWANYO WA MAPATO YATOKANAYO NA MKUHUMI UNAOENDESWA NA CHUO KIKUU ARDHI NA KUSIMAMIWA NA CHUO KIKUU CHA KILIMO CHA SOKOINE KWA UFADHILI WA SERIKALI YA NORWAY.**

## TIMU YA WATAFITI


1. DK. RIZIKI SHEMDOE – KIONGOZI WA UTAFITI – CHUO KIKUU ARDHI
2. DK. FELISTER MOMBO – MJUMBE – CHUO KIKUU CHA KILIMO SOKOINE
3. DK. DEUSDEDIT KIBASSA – MJUMBE – CHUO KIKUU ARDHI
4. BW. EBENEZER MSHANA – MJUMBE – CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM
5. BW. STEPHANO KINGAZI – MJUMBE – CHUO KIKUU CHA KILIMO SOKOINE

**KWA MASWALI WASILIANA NA**:
KIONGOZI WA UTAFITI
S.L.P 35124, DAR ES SALAAM
SIMU: +255 22 2775481
BARUAPEPE: shemdos@gmail.com

## UTANGULIZI

MKUHUMI MAANA YAKE NI MPANGO WA KUPUNGUZA UZALISHAJI WA HEWA UKAA KUTOKANA NA UKATAJI MITI HOVYO NA UHARIBIFU WA MISITU AMA KWA LUGHA YA KIGENI "REDUCED EMMISSION FROM DEFORESTATION AND FOREST DEGRADATION AU (REDD) KWA KIFUPI.

MKUHUMI NI MRADI ULIOIBULIWA NA UMOJA WA MATAIFA KWA MADHUMUNI YA KUDHIBITI UKATAJI MITI ILI KUSAIDIA KUPUNGUZA ATHARI ZA MABADILIKO YA TABIA NCHI. ILI MISITU IWEZE KUKAA BILA KUKATWA INABIDI BAADHI YA WATU HASA WA MAENEO YA VIJIJINI, WAPUNGUZE MATUMIZI YA NISHATI ZA KUNI, NA MKAA PAMOJA NA MIJENGO NA HATA MBAO ZA KUTENGENEZEA SAMANI ZA MAJUMBANI. HII NI KUTOKANA NA TAFITI KUONYESHA KUWA MATUMIZI HAYA YAMECHANGIA KWA KIASI KIKUBWA KATIKA KUHARIBU MISITU NA KULETA MABADILIKO YA TABIA NCHI. KWA KUFANYA HIVYO INA MAANA

JAMII HIYO ITAINGIA KATIKA GHARAMA FULANI.

MKUHUMI ULIANZA KUZUNGUMZWA KATIKA MIKUTANO MBALIMBALI YA KIDUNIA YA MAZINGIRA KUANZIA ULE WA MWAKA 2005 ULIOFAHAMIKA KAMA COP 11. MICHAKATO KADHAA YA KUJADILI AJENDA YA MKUHUMI KATIKA NGAZI YA KIDUNIA ILIYOJUMUISHA MIKUTANO MBALIMBALI YA WATAALAMU WA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI ILIENDELEA KUFANYIKA KATI YA MWAKA 2005 NA 2006 IKIWEMO ILE ILIYOANDALIWA NA SHIRIKA LA UMOJA WA MATAIFA LINALOSHUGHULIKIA MABADIRIKO YA TABIA NCHI YAANI UNFCCC.

LENGO KUU LA MKUHUMI LILIKUWA NI KUHIFADHI HEWA UKAA KATIKA MISITU KWA KUIONDOSHA KATIKA ANGA. LENGO JINGINE LILIKUWA NI KUZIWEZESHA JAMII ZINAZOISHI KATIKA MAENEO YA MISITU KUNUFAIKA NA FAIDA NYINGINEZO NYINGI

AMBAZO ZINGETOKANA NA MKUHUMI. LAKINI FAIDA ILIYO KUBWA ILIKUWA NI KUZIWEKEZA JAMII ZITAKAZOKUWA ZINATUNZA MISITU KUJIPATIA MAPATO YATAKAYOTOKANA NA KUUZA HEWA UKAA ITAKAYOKUWA IMEONDOLEWA KATIKA ANGA NA KUHIFADHIWA KATIKA MISITU YAO. KWA MANTIKI HIYO MISITU INGESTAWI ZAIDI NA KUIMARIKA NA HIVYO KUONGEZA UTUNZAJI WA MAZINGIRA NA KUPUNGUZA KWA KIASI KIKUBWA ATHARI ZA MABADILIKO YA TABIA NCHI.

BAADA YA MKUHUMI KUWA NI AJENDA ILIYOKUBALIKA DUNIA NZIMA, MNAMO MWAKA 2009 SERIKALI ZA TANZANIA NA NORWAY ZILIKUBALIANA KUFANYA MIRADI YA MAJARIBIO NCHINI TANZANIA KWA KUSHIRIKISHA WADAU MBALIMBALI WAKIWEMO WANANCHI WANAOISHI MAENEO YENYE MISITU, MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI YAANI NGO’S NA VYUO VIKUU PAMOJA NA MAMLAKA YA HALI YA HEWA (TMA) AMBAVYO KWA PAMOJA VILIJIKITA ZAIDI KATIKA KUFANYA

TAFITI.

CHUO KIKUU ARDHI (ARU) NI MOJAWAPO YA VYUO VILIVYOSHIRIKISHWA PAMOJA NA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM (UDSM) NA CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO (SUA). MOJA YA TAFITI ZILIOFANYWA NA CHUO KIKUU ARDHI KWA KUSHIRIKIANA NA WATAFITI KUTOKA VYUO VIKUU VYA DAR ES SALAAM NA SOKOINE NI HUU ULIOLENGA KUPATA MFUMO ULIO BORA WA MALIPO NA MGAWANYO WA FAIDA MBALIMBALI ZITOKANAZO NA BIASHARA YA HEWA UKAA KATIKA MAENEO MBALIMBALI YA MIRADI YA MAJARIBIANO KAMA NJIA MBADALA YA KUJIONGEZEA KIPATO NA KUTUNZA MAZINGIRA.

**LENGO KUU LA UTAFITI**

UTAFITI HUU ULIIBULIWA KUTOKANA NA UKOSEFU WA MFUMO WA KUELEWEKA UTAKAOTUMIKA KATIKA MGAWANYO WA FAIDA MBALIMBALI ZITOKANAZO NA MKUHUMI IKIWEMO FEDHA

ZITAKAZOTOKANA NA KUUZA HEWA UKAA NCHINI TANZANIA. KUTOKANA NA SABABU HIYO UTAFITI HUU ULILENGA KUUNDA MFUMO UTAKAOKUWA UMEPATIKANA KWA NJIA SHIRIKISHI AMBAO UTAPENDEKEZWA KWA SERIKALI ILI UTUMIKE KATIKA MGAWANYO WA FAIDA MBALIMBALI ZITAKAZOTOKANA NA MKUHUMI KWA SIKU ZA MBELENI. HII ILITOKANA NA UKWELI KWAMBA MIRADI YA MKUHUMI INGEENDELEA NA KUPATA MAFANIKIO PALE TU AMBAPO WANANCHI WANGEONA FAIDA ZA MOJA KWA MOJA AMBAZO PAMOJA NA MAMBO MENGINE ZINGEKUWA CHACHU YA KUBORESHA MAISHA YAO YA KILA SIKU.

**MALENGO MADOGOMADOGO YALIKUWA NI**

1. KUPIMA MWAMKO NA MTIZAMO WA JAMII KATIKA KUTEKELEZA MIRADI YA MKUHUMI,

2. KUCHAMBUA MIFUMO MBALIMBALI YA MGAWANYO WA FAIDA

INAYOTUMIWA NA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI KATIKA MIRADI YA MAJARIBIO YA MKUHUMI ILI KUJUA VIGEZO VITAKAVYOTUMIKA KATIKA MGAWANYO WA FAIDA,

3. KUCHAMBUA NAFASI YA UMILIKAJI WA ARDHI KATIKA MGAWANYO WA FAIDA ZA MKUHUMI

UTAFITI HUU ULILENGA PIA KUONGEZA UFAHAMU JUU YA MASUALA YA MKUHUMU NCHINI TANZANIA KWA KUFANYA MIKUTANO NA WANAVIJIJI NA WADAU WENGINE NA PIA KUTENGENEZA MACHAPISHO MBALIMBALI NA KUYASAMBAZA SEHEMU MBALIMBALI DUNIANI KWA KUPITIA MAJARIDA YA KITAALUMA. LAKINI PAMOJA NA HAYO, HATUPASWI KUSAHAU KWAMBA MADHUMUNI MAKUBWA YA MKUHUMI YALIKUWA NI KUPUNGUZA HEWA UKAA AMBAYO IMESABABISHA MABADILIKO YA TABIA NCHI YALIYOLETA MADHARA NA

MAAFA MBALIMBALI KATIKA MAENEO MENGI DUNIANI.

MIRADI YA MAJARIBIO YA MKUHUMU ILIKUWA IKIENDESHWA KATIKA VIJIJI MBALIMBALI NCHINI TANZANIA VILIVYOKUWA VINAJIHUSISHA NA UTUNZAJI WA MISITU. KATI YA VIJIJI HIVYO UTAFITI HUU ULILENGA VIJIJI KUMI NA NNE (14) TANZANIA NZIMA. UTAFITI HUU PIA ULISHIRIKISHA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI YANAYOENDESHA MIRADI MBALIMBALI YA MKUHUMI KATIKA VIJIJI HIVYO KUMI NA NNE (14). JEDWALI LINALOFUATA LINAONYESHA VIJIJI NA MASHIRIKA YANAYOFANYA KAZI KATIKA VIJIJI HIVYO.

## JEDWALI 1: VIJIJI VILIVYOTEMBELEWA KWA UTAFITI

| NA | JINA LA KIJIJI | WILAYA | MKOA | SHIRIKA LINALOFANYA KAZI MAENEO HAYO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MASANGE | KONDOA | DODOMA | AFRICAN WILDLIFE FOUNDATION (AWF) |
| 2. | ITUNDWI | | | |
| 3. | MANYADA | SHINYANGA VIJIJINI | SHINYANGA | TATEDO |
| 4. | PANDAGICHIZA | | | |
| 5. | NAMBONDO | KILWA | LINDI | MPINGO CONSERVATION AND DEVELOPMENT INITIATIVES (MCDI) |
| 6. | MANDAWA | | | |
| 7. | MILOLA MAGHARIBI | LINDI MJINI | LINDI | TANZANIA FOREST CONSERVATION GROUP (TFCG) |
| 8. | KINYOPE | LINDI VIJIJINI | | |
| 9. | ILAGALA | KIGOMA VIJIJINI | KIGOMA | JANE GOODALL INSTITUTE (JGI) |
| 10. | KARAGO | | | |
| 11. | ILOLO | RUNGWE | MBEYA | WILDLIFE CONSERVATION SOCIETY (WCS) |
| 12. | KIBISI | | | |
| 13. | CHARAWE | KATI | KUSINI UNGUJA, ZANZIBAR | CARE - TANZANIA |
| 14. | MUYUNI C | KUSINI | | |

KUTOKANA NA UMUHIMU WA KUPATA MFUMO ULIO BORA WA MGAWANYO WA FAIDA MBALIMBALI ZITOKANAZO NA MKUHUMI NA ULIOPATIKANA KATIKA NJIA ILIYO SHIRIKISHI, VIJIJI NA MSHIRIKA YALIYOTAJWA HAPO JUU PAMOJA NA WADAU WENGINE WA MKUHUMI WALISHIRIKISHWA KATIKA UKUSANYAJI WA TAARIFA NA MAPENDEKEZO MBALIMBALI KATIKA KUTENGENEZA MFUMO HUO. NJIA ZILIZOTUMIKA KUKUSANYA TAARIFA KUTOKA KWA WADAU MBALIMBALI NI; MAHOJIANO KATIKA VIKUNDI VIDOGO VIDOGO NA MAHOJIANO YA MTU MMOJA MOJA KWA KUTUMIA MADODOSO AMBAPO JUMLA YA KAYA 615 WALIHOJIWA.



*WANAKIJIJI CHA ITUNDWI WILAYANI KONDOA MKOANI DODOMA WAKIWA KATIKA MAHOJIANO YA VIKUNDI VIDOGOVIDOGO WAKATI WA UKUSANYAJI WA TAARIFA ZA UTAFITI*

## MATOKEO YA UTAFITI

MATOKEO YA UTAFITI HUU NI MAPENDEKEZO YA MGAWANYO WA MAPATO UTAKAOFAA KWA JAMII ZOTE ZA TANZANIA HUKU UKILENGA KUNUFAISHA WADAU WOTE WANAOHUSIKA KATIKA BIASHARA YA HEWA UKAA.

## MAMBO MAKUU YA KUZINGATIA KATIKA MAPENDEKEZO HAYO NI;

I. KUHAKIKISHA KUWA MUUNDO WA SERIKALI UNAHUSISHWA KWA AJILI YA KUFANYA MKUHUMI KUWA ENDELEVU,

II. KUWE NA UWAZI KATIKA MGAWANYO WA FEDHA ZITAKAZO TOKANA NA KUUZWA KWA KABONI,

**MAPENDEKEZO HAYO NI KAMA IFUATAVYO.**

## PENDEKEZO LA KWANZA: KWA MSITU UNAOSIMAMIWA KWA PAMOJA KATI YA JAMII NA SERIKALI (PFM)

**MGAWANYO WA MAPATO UZINGATIE YAFUATAYO:**

I. MIRADI YA KIJAMII YA MAENDELEO,

II. SHUGHULI MBADALA ZA KUONGEZA KIPATO,

III. FEDHA KWA AJILI YA KUZUIA SHUGHULI ZA UKATAJI MITI OVYO NA UHARIBIFU WA MISITU,

IV. KILA ENEO/KIJIJI KITAHITAJIKA KURIDHIA NI KIASI GANI CHA FEDHA KIPELEKWA KWENYE MAENEO HAYA MATATU NA MARIDHIANO HAYO YATAPITISHWA NA MKUTANO MKUU WA KIJIJI.



*UPIKAJI KWA KUTUMIA BAYOANUAI ASILIA WILAYANI SHINYANGA VIJIJINI, MOJA KATI YA FAIDA ZILIZOTOKANA NA MRADI WA MKUHUMI UNAOENDESHWA NA SHIRIKA LA TATEDO ILI KUPUNGUZA UHARIBIFU WA MISITU.*

## PENDEKEZO LA PILI:
## KWA MSITU UNAOSIMAMIWA NA JAMII (CBFM)

I. FEDHA ZA KUSHUGHULIKIA URATIBU NA UPIMAJI WA KABONI ITENGWE NA KUPELEKWA WILAYANI MOJA KWA MOJA

II. KIASI KIKUBWA CHA FEDHA ZINAZOTOKANA NA UUZAJI WA

KABONI ZIPELEKWE VIJIJINI KUPITIA HALMASHAURI ZA VIJIJI NA MGAWANYO UTATEGEMEA NA NAMBA YA HALMASHAURI ZA VIJIJI VINAVYOSIMAMIA MSITU HUO

III. MKUTANO MKUU WA KIJIJI UTAAMUA MATUMIZI YA FEDHA ITOKANAYO NA KABONI ITAKAYOKUWA IMEPELEKWA KATIKA KIJIJI HUSIKA

IV. MAAMUZI YA KIASI GANI KIENDE WAPI YAFANYWE NA HALMASHAURI YA KIJIJI NA KUIDHINISHWA NA MKUTANO MKUU WA KIJIJI



*UKULIMA BORA WA ALIZETI KATIKA KIJIJI CHA MASANGE WILAYANI KONDOA MKOANI DODOMA KAMA NJIA MBADALA YA KUJIONGEZEA KIPATO NA KUPUNGUZA UTEGEMEZI KATIKA MISITU*

MAPENDEKEZO HAYA YALIYOTOKANA NA UTAFITI HUU YAMESAMBAZWA KWA WADAU MBALIMBALI KATIKA NGAZI YA KITAIFA NA KIMATAIFA KAMA IFUATAVYO:

1. YALIWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA MAZINGIRA WA DUNIA YAANI COP 18 ULIOFANYIKA HUKO DOHA,

2. YALIWASILISHWA MBELE YA WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA KIMATAIFA ULIOANYIKA JIJINI TOKYO NCHINI JAPAN,

3. KATIKA NGAZI YA KITAIFA MATOKEO HAYA YALIWASILISHWA

4. KATIKA MKUTANO WA WABUNGE WA KAMATI YA ARDHI NA MAZINGIRA ULIOFANYIKA HUKO DODOMA MWAKA 2013,

5. NA PIA KWENYE MIKUTANO MBALI MBALI YA KITAFITI YA MKUHUMI.

SEHEMU YA MATOKEO HAYA YALITUMIKA KATIKA MAENEO MBALIMBALI KAMA IFUATAVYO:

1. KATIKA MCHAKATO UNAOENDELEA WA KUUNDA MFUKO WA KITAIFA WA KUSAIDIA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI YAANI

KWA LUGHA YA KIGENI "CLIMATE CHANGE FINANCING MECHANISM",

2. KATIKA MCHAKATO WA KUANDAA MIONGOZO YAANI "GUIDELINES" ZA MALIPO YA FEDHA ZA MKUHUMI, ANDIKO AMBALO LINASIMAMIWA NA SHIRIKA LA MAENDELEO LA UMOJA WA MATAIFA YAANI UNDP KWA NIABA YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII.

UTAFITI HUU PIA UMECHANGIA KWA KIASI KIKUBWA KATIKA KUANDAA WATAALAMU WA MAZINGIRA NA MABADIRIKO YA TABIA NCHI KATIKA NGAZI YA SHAHADA YA UZAMILI KAMA MTAKAVYOWASIKIA HAPO BAADAE. KWA UJUMLA WAKE, UTAFITI HUU UMEONGEZA UFAHAMU WA MASUALA MBALIMBALI YANAYOHUSU MKUHUMI KWA WANAVIJIJI NA WADAU MBALIMBALI KUPITIA MIKUTANO MBALIMBALI AMBAYO ILIENDESHWA VIJIJINI. JAMII YA WANATAALUMA IMENUFAIKA PIA KUPITIA MACHAPISHO MBALIMBALI YALIYOTOKANA

NA UTAFITI HUU. KWA MANTIKI HIYO INAONYESHA NI JINSI GANI UTAFITI HUU ULIKUWA MUHIMU NA UMEKUJA KWA WAKATI MUAFAKA KWA CHUO CHETU KAMA WATAFITI, KWA WADAU MBALIMBALI WA MKUHUMI NA KWA TAIFA KWA UJUMLA.

## HITIMISHO

KWA KUMALIZIA, CHUO KIKUU ARDHI KINATAMBUA NA KUTHAMINI MCHANGO MKUBWA ULIOTOLEWA NA VIJIJI NA MASHIRIKA MBALIMBALI YASIYO YA KISERIKALI PAMOJA NA WADAU WENGINE. SHUKRANI ZA PEKEE ZIENDE KWA SERIKALI YA NORWAY KWA KUWEZESHA UPATIKANAJI WA FEDHA KWA AJILI YA UTAFITI HUU NA CHUO KIKUU CHA KILIMO CHA SOKOINE KWA URATIBU WA MIRADI YOTE YA MKUHUMI.

***IMEANDALIWA NA:****DR. DEUSDEDIT KIBASSA*
***IMESANIFIWA NA:****MS. BERTHA SAMBO*